# NEEMA YA KUNYAKULIWA – IMANI YA KUNYAKULIWA

*I Petro 1:13: Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi, mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo.*

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alivyosema juu ya hilo:

Hiyo ndiyo sababu ninaamini kwamba wakati Bibi arusi atakapoitwa atoke na kuchaguliwa na awekwe sawa kwenye kitabu cha uzima, utakuja uvumi wa sauti kutoka Mbinguni ambao utachukua ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya Bibi Arusi ambao utamchukua Bibi Arusi kutoka duniani katika Neema ya kunyakuliwa Mungu aliahidi hilo.

Sijali ni sayansi ngapi au ni wana anga wangapi wametia saini zao, na kitu kingine chochote, na wanaweza kuona maili ngapi, sijali chochote juu ya hilo. Ziko Mbingu na yuko Yesu Kristo halisi pale ambaye atakuja katika umbo la kimwili kulipokea Kanisa lake na Bibi Arusi!
(1 Wathesalonike 4:16-17). Haijalishi hiyo hadithi inaonekana ni ya kizamani, bado ni ya kweli, Mungu alisema hivyo. Hivyo ndivyo waaminio wanavyoamini. [1]

Ninaamini kweli, ninaamini, kabla ya Kanisa kuwa na unyakuo, lazima liwe na imani ya kunyakuliwa. Hatuna Imani ya kutuponya kiungu ukiachilia mbali imani ya kunyakuliwa tunapaswa kuwa na Imani ambayo itatubadilisha na kuhuisha miili, na kuchukuliwa mbali (1Kor. 15:51-54) Ninaamini liko Kanisa njiani, usiku huu wa leo, nguvu ya Mungu aliye hai, ambapo wanaume watanena Neno hapa na pale, na litawaka kama umeme. Na Kanisa linakuja, sio saikolojia, siyo vitu hivi vya kujifanya, imani bandia, Lakini ni halisi ya kweli, iliyopakwa mafuta na Roho Mtakatifu, Kanisa lililoitwa. Amen. [2]

Na zungumzia juu ya Kanisa kwa ajili ya Neema ya unyakuo, litakuja kuwepo tutakapozivunja chini Kanuni zetu, tusahau mambo yetu yote ya kidhehebu na kuja kwenye msingi wa Neno la Mungu. [3]

Wako hapo wanawali wako watano wenye busara wakiwa na mafuta katika taa zao, Imani ya kunyakuliwa, kuamini Ishara zote, maajabu, unabii na kila kitu. Na hawa watano waliokatwa kutoka kwenye mabaki walichukuliwa mbali. Na wale wote waliobaki walikuwa bado ni mabikira na hawatapotea, lakini wataingia kwenye dhiki kuu. Yesu alisema “Itakuwapo ….” (Matayo 25:1-13). Na wakasema. Tupeni mafuta yenu kidogo, “tunataka Roho Mtakatifu sasa”. [4]



Na, ninataka ninyi mjengeke sasa katika maneno Matakatifu ya Mungu, katika Imani, Imani ya saa hii. Ile Imani, itahitajika Imani zaidi kuliko wakati mwingine wowote, kwa maana ni lazima iwe Imani ya kunyakuliwa, kuchukuliwa juu
(Yuda 3). [5]

Sasa, Mwalimu mkuu, kama ulivyotufundisha sisi katika Neno lako lililo zuri sana, mioyo yetu inatetemeka kwa Neema ya kunyakuliwa kujua kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, (Yohana 5:24). Yote ni kwa sababu ya uzuri wa Bwana Yesu aliyetuita sisi, na ametuosha sisi katika damu yake, na ametuwakilisha sisi mbele ya kiti cha enzi cha Mungu tusio na mawazo, tusio na lawama, kwa maana alichukua dhambi zetu, hatuna dhambi. Mungu amemtwika Yeye maovu yetu yote juu yake na alijeruhiwa kwa makosa yetu (Isaya 53:4-7). Oh, jinsi tunavyompenda yeye, Yule Mwana Kondoo mkubwa wa Mungu. [6]

Kama tu tunavyojua sasa, kama mtu mmoja alivyoniuliza muda mfupi tu uliopita juu ya kule kuja na kule kunyakuliwa. Tunajua tumeishi huo wakati na umeisha wakati wa unyakuo uko karibu. Na tunaangalia ile Imani ya kunyakuliwa ambayo itayasukuma Makanisa pamoja na kuyapa ile nguvu ya kimiujiza ambayo itageuza miili hii ambayo tunaishi ndani yake. (Wafilipi 3:20-21).

Tunamuona Mungu ambaye anawainua wafu kutoka mavumbini, au nje kule uwanjani, na kuwapa tena uzima, na kumuwakilisha mbele yetu. Tunapomuona Mungu ambaye anaweza kuondoa kensa ambayo imemtafuna mtu hata akawa ni kivuli tu, na kumwinua kumuweka kwenye afya kamili, hiyo inapaswa kuwapa watu imani ya kunyakuliwa. Kwamba hiyo nuru itakapoangaza kutoka mawinguni, na tarumbeta ikilia, ule mwili wa kristo utakusanywa pamoja haraka, na kubadilishwa mara moja, na kuchukuliwa Mbinguni juu. [7]

Na mwishoni mwa wakati wa Pentecoste tunapaswa kupokea kutokana na Neno, na Mungu aniwezeshe mimi usiku wa leo niwaonyeshe kupitia hapa, kwamba tutapokea mjumbe ambaye atachukua sehemu hizi zote zilizoachwa nje kule na afunue siri zote za Mungu kwa ajili ya kunyakuliwa kwa Kanisa. Na baadaye kunakuja ngurumo saba za siri ambazo hata hazikuandikwa. Hiyo ni kweli. Na ninaamini kwa kupitia hizo ngurumo saba zitakazofunuliwa wakati wa mwisho ili kumleta Bibi Arusi pamoja; kwa sababu tulichonacho sasa, hatuwezi kufanya hilo. Kuna kitu fulani tunapaswa kupiga hatua zaidi, kwa shida sana hatuwezi kupata Imani ya kutosha kwa uponyaji wa kiungu.

Inatupasa tuwe na Imani ya kutosha ili kubadilishwa katika muda mfupi na kunyakuliwa juu mbali na dunia hii, na tutaliona hilo baada ya muda, Mungu alipenda, tuone limeandikwa wapi.

Lakini fikiri, sasa ameandika hili, lakini alipoanza kuandika hizo ngurumo saba nyingine, alisema, “Usiandike hayo” aliagizwa kuandika kila kitu alichokiona. Lakini wakati hizi ngurumo saba za ufunuo 10 zilipotoa sauti zao, alisema, “Usiandike hizo hata kidogo” (Ufunuo 10:1-7). Ni siri. Bado hatujajua ni nini,

lakini kwa mawazo yangu zote zitafunuliwa. Na zitakapo fanyika hivyo, itatupa Imani kwa ajili ya Neema ya kunyakuliwa kwa ajili ya Kanisa kuondoka. Tunajaribu kusogea katika kila kitu tunachokijua, kupitia nyakati mbali mbali tumeangalia kila kitu. Tumeona siri za Mungu. Tumeona kule kuonekana kwa kusanyiko kubwa la pamoja la Bibi Arusi katika siku za mwisho, lakini bado kuna kitu pale ambacho hatuwezi kuona sisi bado. Kuna kitu fulani na fulani. Lakini ninawazia wakati hizo siri zitakapoanza kuja … Mungu alisema, zuilia hayo usiyaandike sasa. Ngoja kidogo. Nitayafunua katika siku ile, usiiyaandike hata kidogo, Yohana, kwa sababu yatawatia bumbuazi hayo, yaachilie. Lakini nitayafunua hayo katika siku za mwisho itakapohitajika yafanyiwe hivyo". [8]

Na Baba, mambo mengi yanaweza yakasemwa hapa sasa hivi, Pengine Kanisa halitaelewa. Lakini naomba uwape shauku kuu juu ya hayo, Bwana, kwamba wangekuja na kuona kwamba tuko wakati wa mwisho, wakati wa wana anga. Ninaomba, Baba, kwamba watafahamu kwamba sio kujaribu kuwahukumu kwa kile walicho nacho, ni kujaribu kuwapa Neema zaidi ya kunyakuliwa. Kwa maana saa inakuja ambapo lazima tuwe na nguvu ya kunyakuliwa, sio tu ya kuponya mwili lakini kuubadilisha huo katika muda wa kufumba na kufumbua. Kristo atakuwa halisi katika miili yao (Wakolosai 1:24-29), mpaka anaweza kuibadilisha hiyo kwa kifo chake kikuu na kile alichokinunua. Hebu walichukue hili leo, ile ishara niliyozungumzia usiku wa jana, ishikilie mbele yao na watembee kuja kwa huyu mwana anga. (Tupe hilo, Baba), ambapo maono, nguvu, na dunia ng'ambo ya zijulikanazo, na D Mungu, ambapo siri zote kuu za Mungu zinafunuliwa katika hii mihuri saba na kufanya ijulikane kwa wanadamu. Tujalie hilo Baba. [9]

Ni ya kitakatifu sana kwamba sipaswi kunena mengi juu ya hilo, kama alivyoniambia pale mwanzoni. Alisema, "Hili usiseme chochote juu yake". Mnakumbuka hilo miaka mingi iliyopita? Linajinenea lenyewe. Nimejaribu kuwaelezea yale mengine, na nilifanya makosa. Hii itakuwa ni kile kitu kwa mawazo yangu (sisemi Mungu ameniambia hilo)… hii itakuwa ni kile kitu kitakachoanzisha Imani ya kunyakuliwa ili kuondoka. Sasa, na hilo…. Inanipasa nikae kimya kwa muda kidogo. [10]

Hatte wright, siku ile, hakuomba kitu chochote. Yeye alikuwa tu amekaa pale, Lakini alisema neno lililosahihi, ambalo lilimpendeza Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu akazungumza na kumwambia, "Hattie, Omba lolote utakalo, chochote ulicho nacho na unachohitaji. Uliza uone kama hili ni kweli au sio. Omba lolote (Uponyaji wa dada yake kiwete aliyekaa pale na miguu iliyopooza, Dollar elfu kumi asiendelee tena kulima katika milima ile, arudishiwe ujana wa mwili wake uliozeeka). Chochote utakachoomba, kiombe sasa hivi, Kama hakitatendeka na nikupe sasa hivi, kama sivyo mimi ni nabii wa uongo". Hilo ni jambo hasa, si ndiyo?

Yesu alisema, "Uambie mlima huu ….." (Marko 11:22-26) Na mmesikia juu ya yale yaliyokuwa yakitokea, hiyo ndiyo huduma tunayoendea sasa, tuko juu kabisa ya barabara sasa. Karibuni kule Kuja kwa Bwana Yesu. Na inabidi tuwe na Imani ya



kunyakuliwa katika Kanisa ambayo itatufanya tubadilishwe kwa kitambo tu kufumba na kufumbua tuondoke au sivyo hatutaenda. Lakini usiwe na wasi wasi, itakuwepo. Itakuwepo nguvu ya Kanisa hili ikiinuka, itawaleta ndugu zao, nguvu ya Kanisa hili ikiinuka itawaleta ndugu zao, Nguvu ya Kanisa lile itawaleta ndugu wengine, hapo sasa kutakuwa na ufufuko wa jumla (ufunuo 20:6) tunaangalia mbele kwa jambo hilo. [11]

Ni Roho Mtakatifu ndiye anayetufanya tuhesabiwe haki. Ninyi wahudumu mnajua hilo, si ndiyo? Roho Mtakatifu anatakasa, Roho Mtakatifu anatujaza sisi, Roho Mtakatifu anatupa Imani ya kunyakuliwa, unaona, kadiri tunavyopanda juu. [9]


**<u>Nukuu za Kiingereza</u>**

[1] Waaminio wa aina tatu Uk. 15
[2] Israeli pale Kadesh Barnea (53-0328, aya 79)
[3] Dunia inamomonyoka vipande vipande 63-1115,Aya 193
[4] Maswali na majibu ya kitabu cha mwanzo 53-0729, COD Uk 53, Aya 260
[5] Chakula cha Kiroho kwa wakati wake, Aya 3
[6] Waebrania sura ya 6 sehemu ya 2 Aya 503
[7] "Mbona unalia, Nena" (63-0714M), Uk. 10
[8] Muhuri wa kwanza Uk. 128+142
[9] Kuhesabu kinyumenyume (64-0209), Aya 95+175
[10] Mtazame Yesu (63-1229E), Uk. 6
[11] Maswali na majibu juu ya Roho Mtakatifu, COD Uk. 411 Aya 20



Jiwe la kiroho la kujengea na. 153 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306


Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)


*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*